SAUTI ZA WATANZANIA

chunguzi kifani juu ya Biashara na Haki za Binadamu

(Toleo la 1)

MUHTASARI JUMUISHI

"Sauti za Watanzania – chunguzi kifani juu ya Biashara na Haki za Binadamu (Toleo la 1)" linaeleza tafiti **tano juu ya mambo muhimu yahusuyo haki za binadamu kwenye mashirika nchini Tanzania** zilizofanywa na Asasi ya Biashara na Haki za Binadamu Tanzania (BHRT), Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (CHRAGG), Asasi ya Governance Links Tanzania, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) na Shirika la IPIS Tanzania.

Chunguzi kifani zinaeleza mambo kadha wa kadha juu ya namna uendeshaji wa biashara unaweza kuathiri haki za binadamu[1], ikiwa ni pamoja na haki za kazi, haki ya kupata afya bora, usalama, uhuru wa kujieleza, uhuru wa kumiliki mali, na kuwa na maisha bora. Wakati ni wajibu wa Serikali *kuwalinda* wananchi dhidi ya ukiukwaji wa haki mahali pa kazi, makampuni yana jukumu la *kuheshimu* haki za binadamu. Hii inamaanisha kwamba yanatakiwa kuwa na uadilifu ili kuepusha ukiukwaji wa haki za binadamu. Ukiukwaji wa haki za binadamu unapotokea, yanatakiwa pia kushughulikia ukiukwaji huu kwa njia sahihi za maridhiano.

Wajibu na majukumu ya serikali na makampuni kuhusu kukabiliana na kushughulikia ukiukwaji wa haki za binadamu kazini umeelezwa kwenye mfumo wa Umoja wa Mataifa, *Miongozo ya Umoja wa Mataifa juu ya Biashara na Haki za Binadamu* (UNGPs)[2]. Serikali zina jukumu kubwa la kutekeleza mfumo huu katika maeneo yao, kwa kutekeleza sera stahiki, sheria na kanuni, kwa kutoa mwongozo na kwa kuweka mbinu maridhawa za maridhiano endapo kumetokea ukiukwaji wa sheria. Hata hivyo, kanuni na usimamizi usio mzuri wa sheria, pamoja na uelewa mdogo wa wananchi, wadau wa biashara na watunga sera, hupunguza kasi ya makampuni kukabiliana na ukiukwaji wa haki za binadamu.

Nchini Tanzania[3], sheria na kanuni zote kwa ujumla zipo kwa ajili ya kulinda haki za msingi za wananchi, kusimamia maslahi ya wafanyakazi na kutunza mazingira ya uendeshaji wa biashara na uwekezaji. Maslahi ya wafanyakazi, kwa mfano, yanasimamiwa na kanuni za kazi kama vile "Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini ya 2004", "Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi ya 2008", "Sheria ya Taasisi za Kazi ya 2004",

1 Haki za msingi kwa wote duniani, kama zilivyotanabaishwa na kuthibitishwa kwenye Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu, Umoja wa Mataifa, 1948. http://www.un.org/en/universal-declaration-human-rights/

2 *Miongozo ya Umoja wa Mataifa juu ya Biashara na Haki za Binadamu: Utekelezaji Mfumo wa 'Kulinda, Kuheshimu na Kupata Unafuu wa Kisheria' wa Umoja wa Mataifa*, Ofisi ya Kamisheni Kuu ya Haki za Binadamu (OHCHR), 2011. https://www.ohchr.org/Documents/Publications/GuidingPrinciplesBusinessHR_EN.pdf

3 Mifano yote ya sheria ni ya upande wa Tanzania Bara. Sheria ya Zanzibar haijatajwa hapa, kwa kuwa chunguzi kifani zote zilifanyikia upande wa Bara wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

"Sheria ya Afya na Usalama wa Wafanyakazi Mahali pa Kazi ya 2003" na "Sheria ya Vyama vya Wafanyakazi ya 1998". Utunzaji wa mazingira unasimamiwa na, pamoja na mambo mengine, "Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya 2004", "Sheria ya Misitu ya 2002" na "Sheria ya Uhifadhi ya Wanyamapori ya 2013". Kwa mfano, Sheria hizi mbili yaani ya Misitu na ya Wanyamapori zinakataza shughuli za binadamu kama vile uchimbaji wa madini, makazi, kilimo na ufugaji ndani ya maeneo ya hifadhi. Haki za ardhi, kwa upande mwingine, zinasimamiwa sanasana na "Sheria ya Ardhi, Na. 4 ya 1999", "Sheria ya Ardhi ya Vijiji, Na. 5 ya 1999" na "Sheria ya Utwaaji wa Ardhi (Sura ya 118, 2002)". Pamoja na mambo mengine, "Sheria ya Utwaaji wa Ardhi" inaainisha mfumo wa utwaaji ardhi wa lazima kwa ajili ya matumizi ya umma kama vile kuweka miundombinu au kutafiti uwepo wa maliasili.

Mbali na sheria, kuna wakala mbalimbali wanaofanya usimamizi, kwa mfano Mamlaka ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi (OSHA). Kinachofurahisha zaidi, Tanzania ina **Taasisi ya Taifa ya Haki za Binadamu** (Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (CHRAGG)) ambayo ni huru na ina meno ya kikatiba kukuza na kulinda haki za binadamu nchini ("Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Na. 7 ya 2001"). Tume hii ina jukumu la kusaidia nchi kuona kama sheria zinazingatia haki za binadamu, kama sheria zinatekelezwa kisawasawa na kama mashirika yote na wadau nje ya serikali wanagawiwa mwongozo wa haki za binadamu. Tume pia ina jukumu la kutoa mwanya wa kufanya maridhiano pale haki za binadamu, ikiwa ni pamoja na zile zinazohusiana na biashara, zinapokuwa zimekiukwa.

Pamoja na mifumo hii rasmi, **bado kuna mapungufu na kukosekana kwa ufanisi** kwenye utekelezaji wa Miongozo ya Umoja wa Mataifa juu ya Biashara na Haki za Binadamu nchini Tanzania, hasa kwenye haki zinazohusiana na kazi, ardhi na mazingira. Hili lilikuwa hitimisho la Tathmini ya Awali ya Kitaifa ya 2017 (NBA)[4] juu ya biashara na haki za binadamu ambayo iliangalia hali ya haki za binadamu kwenye sekta za madini, kilimo na utalii nchini Tanzania. Utafiti wa NBA uligundua kukosekana kwa utekelezaji wa dhati wa haki za binadamu na kutozingatia kanuni za kitaifa na za kimataifa kwenye sekta zote. Mambo mengine yanajitokeza kutokana na ugumu, kukosa ufanisi na kutokuwa na ushikamani kwenye kanuni, pamoja na uelewa mdogo wa wadau wengi juu ya kanuni za msingi za biashara na haki za binadamu.

Katika kukuza uelewa juu ya masuala ya haki za binadamu mahali pa kazi nchini Tanzania, kukuza uelewa na kuboresha ajenda ya taifa juu ya biashara na haki za binadamu, kuna umuhimu wa kufanya tafiti na chambuzi zaidi juu ya mabadiliko ngazi ya taifa na ya chini.

CHUNGUZI KIFANI

Tafiti tano kwenye andiko hili ndo zenye kutujuza leo **chunguzi kifani kutoka sekta kuu nne za uchumi** Tanzania: uchimbaji wa madini, kilimo, utalii, na miundombinu. Mada nyingi za haki za binadamu zinafundishwa, kuanzia kuzingatia masuala ya haki za binadamu kwenye Mradi wa ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki, hadi masuala ya haki za kazi kwenye viwanda vya kuchakata samaki vilivyopo Mwanza na (mashamba ya maua yaliyoko Arusha, hadi mahusiano magumu kati ya wawekezaji wa kwenye utalii na haki za ardhi kwenye Hifadhi ya Taifa ya Saadani, na ule wa kati ya wahifadhi misitu na wachimbaji wa chokaa Mkoa wa Kigoma.

Tafiti kuhusu *"Sauti za Watanzania"* zimegawanyika katika tafiti ndogo ndogo zilizofanyika kwenye maeneo halisi ya kazi zenye lengo la kugusa mambo ya msingi juu ya biashara na haki za binadamu nchini Tanzania. Tafiti zinajumuisha **data mpya za uwandani**, zilizopatikana kwa njia kama usaili kwa wadau, mbinu ya ushuhudiaji au hojaji, pia kupitia data za upili kama mifumo ya sheria za ndani na za kimataifa, ripoti zilizochapishwa au nyaraka za kampuni (sera). Chambuzi za sasa zinaonesha taarifa za nyuma ambazo zilikuwa hazijahifadhiwa kimaandishi, zinatoa picha mpya na **mapendekezo ya wazi** kwa wadau mbalimbali waliohusishwa.

4 *Tathmini ya Awali ya Kitaifa (NBA) ya utekelezaji wa sasa wa mifumo ya biashara na haki za binadamu ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*, THBUB, DIHR & SOMO, Novemba 2017. https://www.humanrights.dk/sites/humanrights.dk/files/media/dokumenter/projects_docs/tanzania_bhr_nba_final_nov2017.pdf

Picha ya mada zilizo kwenye chapisho la "Sauti za Watanzania – chunguzi kifani juu ya Biashara na Haki za Binadamu (Toleo la 1)"

UTAFITI WA 1:

Masuala ya Haki za Binadamu ya kuangalia kwenye Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki upande wa Tanzania *(Asasi ya Governance Links Tanzania)*

Kwenye utekelezaji wao, miradi mingi ya miundombinu unagusa haki nyingi za msingi za binadamu, ikiwa ni pamoja na haki za wafanyakazi, haki za kumiliki mali, haki ya kupata usalama na afya njema mahali pa kazi, pamoja na haki ya kupata fidia kamili endapo haki zimeminywa. Kwa kuzingatia ukubwa wa tatizo na mlolongo wa mambo kwenye Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki – bomba lenye urefu wa km 1,149 linalopitia mikoa nane kaskazini mwa Tanzania -, na linahusisha watanzania na wadau wengine wa kimataifa, mradi huu unaibua fikra katika kukuza uelewa kwenye masuala ya ***haki za binadamu ambazo makampuni yanatakiwa kuzingatia kwenye miradi ya miundombinu****.*

Kadri shughuli za biashara zinavyopanuka kwenye sekta binafsi, **athari chanya na hasi kwenye jamii** nazo huongezeka. Wakati mashirika ya kimataifa yanaweza kuchangia kwenye uchumi na ajira – na hivyo kuchangia kwenye kufurahia haki za binadamu -, mashirika haya pia yanaweza kuleta athari upande wa haki za binadamu wakati wa utendaji kazi wao. Athari chanya na hasi ambazo zinaweza kuathiri haki za binadamu, na hivyo kammpuni zina wajibu wa kuheshimu haki za binadamu, zinatambulika na kuonekana kimataifa, kwa mfano Miongozo ya Umoja wa Mataifa juu ya Biashara na Haki za Binadamu (UNGPs).

Wakati uelewa juu ya biashara na haki za binadamu unaendelea kukua miongoni mwa makampuni, kukosekana kwa uwezo na motisha katika kufanya biashara kwa kuzingatia Miongozo ya Umoja wa Mataifa juu ya Biashara na Haki za Binadamu bado kunatia shaka sana. Nchini Tanzania, uelewa kuhusu biashara na haki za binadamu baina ya wadau serikalini, kwenye makampuni, asasi za kiraia na jamii bado mdogo. Hili linaonekana dhahiri kwenye Mpango Kazi wa Taifa juu ya Haki za Binadamu wa 2013-2017. Moja ya kazi za ujenzi nchini Tanzania ambapo masuala ya haki za binadamu yamepigiwa upatu ni kwenye ujenzi unaohusisha **miradi mikubwa ya miundombinu**, kwa mfano, nishati. Miradi ya jamii hii ya miundombinu mara nyingi huchukua maeneo makubwa ambayo hugusa makazi ya watu, na mara kadhaa huwa inaambatana na kanuni zisizozingatia maslahi sawia ya kampuni, miundo ya kiutawala na jamii.

Uganda na Tanzania ziliwekeana saini kwa ajili ya ujenzi wa **Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP)** mwezi Mei 2017. Bomba lenye urefu wa km 1,445 km litakuwa bomba namba moja duniani kati ya mabomba yenye kutumia umeme na litasafirisha mafuta ghafi kutoka Kabale Parish Wilayani Hoima magharibi mwa Uganda hadi ghuba ya Chogoleani karibu na bandari ya Tanga mashariki mwa Tanzania. Kwa upande wa Tanzania, bomba ambalo lina urefu wa km 1,149, litapitia mikoa 8 na kwa uchache wilaya 25 kaskazini mwa Tanzania. Kwa kuwa mradi huu wa muundombinu unapitia kwenye jamii mbalimbali zenye mikakati tofauti ya kimaisha, anatakiwa mtu makini kukuza uelewa wa masuala ya biashara na haki za binadamu. Linaweza kusaidia katika kukuza wigo wa makampuni kuepuka kuminya haki za wengine na kukuza mikakati ya kuleta maridhiano mara haki za binadamu zikiukwapo.

Uchunguzi huu kifani unabainisha **mambo mazito na muhimu yahusuyo haki za binadamu** yatakayohitaji kuzingatiwa wakati wa ujenzi wa Bomba, kwa mujibu wa matokeo ya utafiti kuanzia mchakato wa kuweka mipango ya Mradi wa Bomba na usaili kupata mawazo ya wadau ambao walikuwa wamefuatwa kwa usaili na timu za mradi. Kwa mtazamo mpana wa ushauri wa kitaalam, mambo yanayojitokeza na yanatakiwa kuangaliwa kwa umakini kuhusu haki za binadamu kwenye ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki ni pamoja na: midahalo kazini, haki za kumiliki ardhi, kutendewa haki, elimu na kupata teknolojia, mazingira ya kazi na ajira, maisha bora, ushiriki, haki za makundi ya jamii mahali fulani na haki za mazingira.

Mapendekezo ya utafiti ni pamoja na**:**

- Kuhakikisha kuna **taarifa za mradi** juu ya mipango, tathmini, hatari na athari kwa njia mwafaka, zinazowezekana na zenye kutekelezeka na mtu yeyote.
- Kuongeza **ushiriki** wa taasisi nyingi, kama vile serikali, sekta binafsi na asasi za kiraia katika kujihusisha na kutoa kanuni kwa makampuni kuheshimu haki za binadamu. Kwa serikali, ni muhimu kuridhia mbinu ya kushirikiana kati ya taasisi za serikali kuu na za serikali za mtaa.
- Kuhakikisha kwamba **wanawake, wanaume, vijana, na makundi ya wasiojiweza** karibu na bomba wanashirikishwa na kupatiwa fursa ya kufanya maamuzi hatua mbalimbali.
- Kukuza mbinu za **kufanya kazi kwa njia rasmi na zisizo rasmi**, kujenga imani miongoni mwa makundi ya wadau ikiwa ni pamoja na yale yanayowakilisha makundi ya wasiojiweza.
- Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (**CHRAGG**) kuunga mkono taasisi nyingine za serikali kukuza uelewa wa pamoja wa, na uwajibikaji katika uwekezaji husika.
- Wadau wa serikali kuruhusu **usimamizi huru**, hasa kwa kuhusisha asasi za kiraia.

UTAFITI WA 2:

Haki za kazi na wafanyakazi kupata maridhiano kwenye viwanda vya kuchakata samaki jijini Mwanza *(Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora)*

Kwa njia ya mapitio ya maandiko na tafiti za uwandani zilizofanyika kwenye viwanda vitatu vya kuchakata samaki Manispaa ya Mwanza, CHRAGG inatathmini ***utekelezaji wa haki za kazi na maisha bora katika sekta hii ya kilimo****. Inatathmini pia ni kwa kiasi gani wafanyakazi kwenye viwanda vya kuchakata samaki wanapata maridhiano nje ya mahakama. Utafiti huu ukiwa kwa mara ya kwanza umejikita kwenye haki za binadamu kwenye viwanda vya kuchakata samaki nchini Tanzania, mchango wake unang'amua kwa mapana kilichoko kwenye sekta ambayo kumekosekana tafiti kwa muda mrefu. Utafiti unabainisha mambo yenye kuhitaji kutatuliwa kwa haraka na kutoa mapendekezo ya hatua gani zichukuliwe katika kuhakikisha haki za kazi zinasimamiwa na kulindwa, na uzingatiaji wa haki kwa wote.*

Utafiti juu ya wafanyakazi kupata maridhiano kwenye **viwanda vya kuchakata samaki jijini Mwanza**, uliofanyika kuanzia tarehe 7 hadi 12 Oktoba, 2018 ulikusudia kuchunguza utekelezaji wa haki za kazi na maisha bora, kutathmini ni kwa kiasi gani wafanyakazi wanatatua migogoro nje ya mahakama, na kiasi cha fidia wanachopata kufuatia ukiukwaji wa haki za kazi.

Wengi wa **Watoa taarifa** kwenye utafiti huu walikuwa waajiriwa na watumishi kutoka menejimenti za viwanda vitatu vya kuchakata samaki vilivyopo Manispaa ya Mwanza, ambavyo ni Nile Perch Fisheries Limited, Omega Fish Limited, na Tanzania Fish Processors Limited. Jumla ya waajiriwa 11 – wanne (4) wakiwa wanawake na saba (7) wanaume – na saba (7) watumishi wa Menejimenti - mmoja (1) wa kike na sita (6) wanaume – walifanyiwa usaili.

Mbinu iliyotumika kufanya utafiti huu ilihusisha mapitio ya maandiko na vikao na watumishi kutoka Menejimenti za makampuni, Afisa Utumishi Kanda ya Ziwa, Afisa kutoka Tume ya Usuluhishi na Upatanishi – Kanda ya Ziwa, Afisa Uvuvi wa Mkoa na Afisa Tawala wa Mkoa. Usaili pia ulitumia hojaji ambazo zilikuwa zimeandaliwa kupima uelewa wa watumishi kutoka menejimenti na waajiriwa kuhusu mambo ya biashara na haki za binadamu. Mwisho, utafiti ulifanyika kwa njia ya ushuhudiaji wa moja kwa moja kuona mazingira ya kazi na vitendea kazi na upatikanaji wa vifaa kinga.

Utafiti huu ulifanywa kutathmini hali ya biashara na haki za binadamu kwenye viwanda vya kuchakata samaki, na hasa kuona kama **haki za kazi zinafuatwa na kama watu wanapata suluhisho nje ya mahakama**. Hii ilisababishwa na ukweli kwamba, hadi uamuzi unatolewa hakukuwa na utafiti mwingine uliokuwa umefanywa kuona hali ya utoaji haki za kazi kwenye sekta ya uvuvi Tanzania. Tafiti zilizofanywa kwenye sekta nyingine za uchumi nchini, kama vile sekta za uchimbaji, biashara na utaliii, zote zilionesha ukiukwaji wa haki za binadamu, hususan haki za kazi na haki sawa kwa wote.

Hali jumuishi ya haki za kazi kwenye viwanda vitatu vilivyofanyiwa utafiti ni nzuri kwa upande wa kuleta maisha bora, pamoja na mapungufu kadhaa yanayotakiwa kufanyiwa kazi. Hakukuwa na malalamiko kuhusu kutolipwa mishahara, ubaguzi wala kulazimishwa kufanya kazi na/au ajira kwa watoto. Mazingira ya kazi yalikuwa rafiki kwani kulikuwa na usafi wa hali ya juu na vifaa kinga; pia wafanyakazi wanalipwa malipo ya ziada. Hata hivyo, wafanyakazi hawaelewi namna mahesabu yanavyokokotolewa katika kulipa malipo ya ziada, kwani kuna wengine hawapewi nakala za mikataba ya ajira na, hivyo, hawajui masharti ya ajira zao.

Matokeo ya utafiti ni pamoja na uwepo wa **mbinu za ndani za utatuzi wa migogoro** inayojitokeza mahali pa kazi, ikiwa ni pamoja na kuwa na kamati za nidhamu. Mbali na hizo, wanatumia mbinu za utatuzi wa migogoro nje ya mahakama kwa mfano Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA), Mamlaka ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi (OSHA), Kamati za Ofisi za Kazi na vyama vya wafanyakazi kama TUICO zinatumika kumaliza migogoro kazini. Utafiti uligundua kwamba pamoja na kuwepo kwa mbinu za utatuzi, waajiriwa hawazitumii kwa kuwa wanakosa uelewa na njia za kuzifikia. Baadhi ya mbinu hizi zinasaidia kupatikana kwa maridhiano lakini maridhiano yanayotolewa si matazamio ya walioumizwa kwenye migogoro ya kazi. Kwa ujumla, waajiriwa na waajiri hawana elimu ya kutosha kuhusu haki za kazi na maisha bora. Iligundulika zaidi kwamba **mbinu za serikali za utatuzi wa migogoro nje ya mahakama** yaani Tume ya Usuluhishi na Uamuzi na Ofisi ya Kazi, hazitekelezi majukumu yao kwa ufanisi. Zinakosa rasilimali fedha na rasilimali watu.

Utafiti uling'amua zaidi kwamba waajiriwa wengi kwenye sekta ya samaki ni **vibarua** wenye kufanya kazi kwenye ajira za muda mfupi na zisizo salama. Vibarua wengi hawajapewa nakala za mikataba ya ajira zao na wanapokea ujira usioweza kulipa gharama za kawaida za maisha Tanzania.

Mapendekezo muhimu ya utafiti huu:

- **Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu** inashauriwa kupitia upya Agizo la Utoaji wa Mishahara katika Taasisi za Kazi la 2013 (Na. 196/2013) na kuongeza kima cha chini kitakachoendana na gharama za maisha, kuongeza rasilimali kwenye mifumo ya utatuzi migogoro

nje ya mahakama, kuwajengea uwezo wafanyakazi wa viwandani, menejimenti na wengineo juu ya biashara na haki za binadamu.

- Inashauriwa pia **Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii (SSRA)** kufuatilia kwa umakini ili kuona kama mifuko ya jamii inapokea michango kutoka kwa waajiriwa na waajiri.
- Mwisho, **Ofisi ya Kamishna wa Kazi na OSHA** wanaombwa kuhakikisha haki za kazi na maisha bora zinatiliwa mkazo makazini.

UTAFITI WA 3:

Uzingatiaji wa haki za kazi kwenye sekta ya maua Tanzania: uchunguzi kifani wa shamba la maua la Mount Meru *(wilayani ya Arumeru, mkoa wa Arusha) (Biashara na Haki za Binadamu Tanzania)*

Kama ilivyo kwenye sekta ya uvuvi, sekta ya maua Tanzania nayo imesahaulika mara kadhaa kwenye masuala ya haki za binadamu, na hasa haki za kazi. Hata hivyo, ikiwa kama moja ya sekta za usafirishaji bidhaa nje ya nchi zinazokua kwa haraka, athari zinazogusa haki za jamii, mazingira, afya na kazi yanayotokana na uzalishaji maua yanagusa wengi. Data za uwandani juu ya ***uzingatiaji wa haki za kazi na uelewa kuhusu haki za binadamu kwa ujumla wake kwenye shamba la maua la Mount Meru*** *zinatanabaishwa, pia mitazamo ya wadau wengine (wadau wa asasi ya kiraia, jamii ya maeneo husika na serikali) juu ya haki za binadamu kwenye sekta ya maua. Matokeo ya utafiti huu yatasaidia kuongeza uelewa juu ya sheria zilizopo za kazi na kuleta chachu ya waajiri, waajiriwa na wanajamii kupata haki sawa.*

Ripoti hii inatokana na utafiti wa awali uliofanywa na Asasi ya Biashara na Haki za binadamu Tanzania (BHRT) kwenye **sekta ya maua Mkoa wa Arusha** (Mount Meru, wilaya ya Arumeru) kuanzia tarehe 11 hadi 20 Oktoba 2018 kwa kushirikiana na Shirika la IPIS ambao ndiyo walifadhili utafiti huu.

Utafiti huu ulikusudia kupata taarifa na kuchunguza kama **haki za kazi, sheria, sera na kanuni za kazi zinafuatwa kwenye sekta ya maua** Tanzania. Kwa miaka kadhaa sasa, sekta ndogo ya maua Tanzania imesahaulika kwenye tafiti zinazohusu utekelezaji wa haki za kazi kwenye sekta ya kilimo. Hata hivyo, sekta hii ya maua imekumbwa na athari zinazolenga haki za jamii, mazingira, afya na haki za binadamu pamoja na mambo yahusuyo kazi, hasa yanayohitaji kuelezwa na wasomi, watafiti, mashirika yasiyo ya kiserikali na hata serikali yenyewe. Katika kupata taarifa inayokosekana, tulitumia data za kitaamuli na za kitakwimu uwandani kuangalia kama haki za kazi zinafuatwa kwa waajiri na waajiriwa wa Shamba la Maua la Mount Meru (Mkoa wa Arusha, Tanzania). Zaidi ya matokeo haya, **uelewa juu ya haki za binadamu kwa ujumla** miongoni mwa waajiri na waajiriwa kwenye sekta na mitazamo ya wadau, kama vile wadau kutoka kwenye asasi ya kiraia, jamii husika, na serikali ambao wanawakilishwa hapa, kuongeza uelewa wa mambo ya haki za binadamu kwenye sekta ya maua Tanzania.

Kupitia utafiti huu, **tunahitimisha** kwamba kitendo cha kushindwa kutimiza viwango vyote vya ajira kama Sheria ya Tanzania ya Ajira na Mahusiano kazini ya 2004 inavyotaka kinawasababishia hali tete wafanyakazi wa Shamba la Maua la Mount Meru. Iligundulika kwamba kulikuwa na mambo mazuri kwenye shamba la maua, kwa mfano uwepo wa mikataba ya ajira iliyoandikwa kwa Kiswahili (ambayo waajiriwa wengi waliweza kuisoma na kuielewa kirahisi), uwepo wa chama cha wafanyakazi na taarifa ya ujumla juu ya afya na usalama kazini. Kwa upande mwingine, tuligundua kwamba wafanyakazi wanafanya kazi kwa zaidi ya muda unaotakiwa, wanalipwa mishahara duni, na hawana vifaa kinga. Kwa Kwa kuongezea, kiwango cha uelewa kwenye sheria za kazi zilizopo, sera na haki za binadamu kwa ujumla ni kidogo kwa waajiri na waajiriwa.

Matokeo ya utafiti huu yatasaidia kuongeza **uelewa** juu ya sheria za kazi zilizopo na **upatikanaji wa**

haki kwa waajiri, waajiriwa na wanajamii. Utafiti huu ni mwanzo wa kuweka sawa mambo kwa siku zijazo kwenye sekta na kufanikisha walengwa na wanajamii kwa ujumla kufanya mabadiliko ya tabia. Hivyo itasaidia pia kupigania mabadiliko ya sera.

Mapendekezo yetu muhimu ni kwamba:

- Juhudi zifanyike **kuongeza uelewa** juu ya haki za kazi na haki za binadamu kwa wafanyakazi na wanajamii wa maeneo ya shamba la maua la Mount Meru.
- Ni vema Serikali ilazimishe sekta ya maua wawe na **mbinu za kushughulikia malalamiko ya kazi**, yaani taratibu za mashirika za kughuhulikia migogoro ziwepo kwenye makampuni ya maua, kwa mujibu wa Miongozo ya Umoja wa Mataifa juu ya Biashara na Haki za Binadamu.
- **Asasi zisizo za kiserikali** ni vema ziwe mstari wa mbele katika kujenga uelewa wa namna ya wafanyakazi kufikisha malalamiko yao pale haki zao zinapokiukwa.

UTAFITI WA 4:

Utalii na haki za ardhi: uchunguzi kifani wa kijiji kidogo cha Uvinje na Hifadhi ya Taifa ya Saadani *(Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu)*

*Utafiti huu unaangalia kwa mapana **mgogoro wa muda mrefu unaohusu uwekezaji kwenye utalii ndani ya mojawapo ya hifadhi za Taifa za Tanzania.** Lengo lake ni kuchunguza vyanzo vya mgogoro wa ardhi wa muda mrefu kati ya jamii ya Mamlaka za Uvinje na Hifadhi ya Taifa ya Saadani, amabo umekuwepo tangu miaka ya 1990. Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) inatathmini kama kuna haki za ardhi za jamii husika zilifuatwa wakati wa uanzishaji wa Hifadhi ya Taifa ya Saadani, haki zipi za binadamu zilikiukwa kutokana na mgogoro huu na kama au la taratibu za kupatikana kwa haki binadamu zilifuatwa kabla ya uwekezaji huu wa mfano kwenye utalii. Mapendekezo yamewekwa kwa namna bora katika kutatua mgogoro huu wa kipekee na namna ya kufuata taratibu za kuwa na haki za binadamu kabla ya uwekezaji kwenye utalii kwa ujumla kufanyika.*

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, kikishirikiana na Shirika la IPIS, walifanya utafiti wenye lengo la kuona namna uwekezaji kwenye utalii unaweza kuathiri haki za binadamu. Utafiti huu ni wa kifani na unajikita kwenye kuondolewa kwa kijiji kidogo cha Uvinje ambacho kimeungana na uwekezaji (wa utalii) wa Hifadhi ya Taifa ya Saadani. Kwa kupitia utafiti huu, tuliazimia kuchunguza vyanzo vya **mgogoro wa ardhi wa muda mrefu kati ya wanakijiji wa Uvinje na Mamlaka ya Hifadhi ya Taifa ya Saadan**. Mgogoro huu umekuwepo tangu miaka ya 1990 wakati kunatokea mipango ya kulipa hadhi Pori la Akiba la Saadani kuwa Hifadhi ya Taifa ambapo mamlaka ziliona ardhi ya kijiji cha Uvinje kama ya umma, kinyume na mitazamo ya wanakijiji. Pamoja na kuwa kulitokea mazungumzo kadhaa, mgogoro huu bado haujatatuliwa na umeshaleta athari hasi kwa jumuiya ya Uvinje, na si kitisho tu cha kutolewa kwenye ardhi ya mababu zao. Kwa kutumia uchambuzi wa mgogoro huu wa ardhi, lengo letu ni kupendekeza njia sahihi ya kutatua mgogoro huu wa kipekee na kuona taratibu za kuhakikisha uwepo wa haki za binadamu kabla ya uwekezaji kwenye utalii kwa ujumla.

Data zilikusanywa kwa kutumia vyanzo vya msingi na vya upili. Mbinu na zana zilizotumika zilikuwa hojaji, usaili, ushuhudiaji na mapitio ya maandiko. Jumla ya watoa taarifa 160 walihojiwa, ikiwa ni pamoja na wanajamii wa kijiji kidogo cha Uvinje, wawakilishi wa Serikali, watafiti huru na taasisi binafsi.

Matokeo ya muhimu ni: (1) kwamba haki za wanakijiji wa Uvinje hazikufuatwa wakati wa kuanzisha Hifadhi ya Taifa ya Saadani. Wanakijiji wa Uvinje ndio wamiliki halali ya ardhi ya mababu zao – yaani ardhi ambayo ndiyo mada ya mgogoro uliosababishwa na kitendo cha kuipa hadhi Hifadhi ya Taifa

– na wanapaswa kufurahia urithi wa mali yao bila kubughudhiwa kwa namna yoyote; (2) kwamba kesi hii inaonesha jinsi uwekezaji kwenye utalii unaweza kuleta athari hasi kwenye haki za binadamu kama taratibu hazijafuatwa na maeneo muhimu ya kuangalia kwenye kutathmini hasara na namna ya kuziepuka, kama vile tathmini za mazingira na za kijamii yamepuuzwa.

Tuligundua kwamba **Mamlaka ya Hifadhi za Taifa** (TANAPA) ilikiuka agano na jamii ya Uvinje kwa kufanya kijiji kidogo cha Uvinje sehemu ya Pori la Akiba la Saadani wakati wa kuchora ramani kwa ajili ya Pori la Akiba. Matokeo yake, wanakijiji wa Uvinje wakawekwa kando wakati wa mchakato wa kulibadili hadhi Pori la Akiba kuwa Hifadhi ya Taifa, kitu ambacho kinawanyima jamii ya Uvinje haki ya ya umiliki. Zaidi ya hayo, tunaonesha kwamba Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (CHRAGG) iliingilia kati mgogoro huu wa ardhi na kutoa hitimisho linalowatetea wanakijiji wa Uvinje. Hata hivyo, ushauri haujatiliwa maanani.

Mapendekezo ni kwamba:

- Hifadhi ya Taifa ya Saadani (SANAPA) na TANAPA wanapaswa **washirikishe wanajamii** kuanzia miradi ya utalii inapoanzishwa na hivyo kufuata haki za binadamu.
- SANAPA na TANAPA ni vema ibariki na kuyafanyia kazi **mapendekezo ya CHRAGG** na kufuata sheria wakati wa utwaaji ardhi badala ya kuwafukuza ovyo.
- Wizara ya Maliasili na Utalii ni vema ishirikiane na mamlaka za serikali za mitaa katika kufuatilia **malalamiko ya Uvinje juu ya ardhi**. Inatakiwa itatue mgogoro na kuanzisha mfumo thabiti wa kisheria wa kusimamia ulazima wa haki za binadamu kwenye uwekezaji wa utalii.
- TANAPA inaweza **ikaangalia uwezekano wa kupata mibadala** kwa mfano kuwaweka pamoja wafanyakazi wa kwenye utalii na wanajamii kwenye ardhi moja kwa kuangalia mfano bora kutoka Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro.
- CHRAGG ni vema **ifuatile** utekelezaji wa mapendekezo yake juu ya mgogoro.
- **Wanajamii** wanahamasishwa kusimamia haki zao na kuhakikisha wanatumia majukwaa sahihi kwenye kuelezea mambo yanayoathiri haki zao.
- Serikali na Asasi za Kiraia ni vema zikashiriki kwenye **kupigania haki za jamii** na dhana ya kuridhia kwa hiari, kabla na kwa kuelezwa vema.
- Serikali ni vema ikaanzisha mifumo ya usimamizi wa sheria itakayohakikisha **haki za binadamu zinafuatwa** wakati wa uwekezaji kwenye utalii.

UTAFITI WA 5:

Uchimbaji wa madini ya chokaa na masuala ya haki za binadamu Mkoa wa Kigoma: Uchunguzi kifani juu ya jamii zinazojishughulisha na uchimbaji madini ya chokaa Makere *(E. Mawala, Mratibu wa Tafiti na Miradi wa Shirika la IPIS Tanzania)*

Mkoani Kigoma, jamii ninazoishi karibu na machimbo zinategemea sana ardhi na rasilimali kwenye Hifadhi ya Msitu wa Makere kwa ajili ya maisha yao. Hii imesababisha mvutanoi kupanda miongoni mwa mamlaka za misitu, ambazo ndiyo zenye jukumu la kusimamia sheria na kanuni zinazokataza shughuli za kibinadamu kwenye hifadhi. Kwa kuangalia mada na mkoa ambao ulishasahaulika kwenye tafiti juu ya ***uchimbaji, haki za binadamu na uhifadhi****, mchango huu unaonesha ukiukwaji wa haki za binadamu ambao kwa muda mrefu umekuwa hauripotiwi na ambao waathirika wake hawapati suluhisho na fidia kwa haraka.*

Lengo la ripoti hii ni kuonesha changamoto za msingi za haki za binadamu wanazopitia **jamii ya wachimba madini ya chokaa Mkoani Kigoma** (Kaskazini magharibi mwa Tanzania). Jamii hizi zinategemea kwa kiasi kikubwa ardhi na rasilimali kwenye Hifadhi ya Msitu wa Makere kwa ajili ya shughuli za kila siku kama vile uchimbaji madini ya chokaa, kilimo, ukataji miti, uchomaji wa mkaa, na ufugaji. Hili linawaweka kwenye mgogoro na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) ambao wana jukumu la kusimamia sheria na kanuni zinazozuia shughuli za kibinadamu kwenye hifadhi za misitu. Mkoa wa Kigoma mara nyingi unasahaulika kwenye tafiti juu ya uchimbaji, haki za binadamu na utunzaji wa mazingira Tanzania. Chanzo na kiasi cha changamoto hizi za haki za binadamu bado kwa kiasi kikubwa havijajulikana. Mchango wa utafiti huu ni kuziba mapengo ya uelewa kwa kutumia uchunguzi linganifu juu ya jamii zinazochimba madini ya chokaa Makere, Kigoma.

Katika kupata mambo haya kwa mapana, **utafiti** ulifanyika kuanzia Septemba hadi Novemba 2018 na ulitumia data za msingi na za upili, ikiwa ni pamoja na usaili na hojaji walizofanyiwa wadau, majadiliano ya kikundi lengwa na kutembelea machimbo. Ripoti hii inagusa mambo muhimu zaidi, na matokeo ya utafiti huu yasichukuliwe kama hitimisho toshelevu.

Ripoti inaonesha **-mvutano kati ya jamii zinazojighughulisha na uchimbaji madini ya chokaa Makere na mamlaka za hifadhi ya msitu** zinatokana na utekelezaji wenye mapungufu wa mifumo ya kisheria ya kusimamia madini na kutowajibika vema kwa mamlaka. Sababu nyingine kubwa ni kuwatumia wakimbizi kutoka kwenye Kambi ya jirani ya Nyarugusu katika shughuli za uchimbaji madini ya chokaa. Mvutano kati ya wachimbaji na mamlaka za msitu wa Makere umekuwa gumzo na kusababisha changamoto kubwa za haki za binadamu. Utafiti huu uligundua matumizi makubwa ya nguvu kupita kiasi kwa wachimbaji (kama vile vipigo na mateso), rushwa, na ukamataji usiozingatia sheria, unyang'anyi na uharibifu wa mali binafsi.

Ukiukwaji mwingi **wa haki hauripotiwi** na waathirika wana uwezekano mdogo wa kupata suluhisho na fidia.

Mapendekezo ni kwamba**:**

- Wadau husika ni vema wachukue juhudi maalum za **kuwajengea uwezo** wachimbaji wa madini ya chokaa ili kuwapa uelewa wa taratibu za kufuata wakati wanajishughulisha na uchimbaji kwenye maeneo yaliyo kwenye hifadhi za misitu.
- Mamlaka za madini na misitu ni vema **zikaungana katika kusimamia mamlaka zao** ili kuweka uwiano kati ya uchimbaji maliasili na uhifadhi wa misitu. Wakishindwa hapo maana yake watakuwa wanaongeza mvutano zaidi kati ya wachimbaji na huduma za misitu Makere, vile vile kwenye hifadhi nyingine za misitu.

HITIMISHO JUMUISHI NA MAPENDEKEZO

Kama ambavyo imeelezwa kinagaubaga kupitia chunguzi kifani zote tano, bila kujali sekta, shughuli za biashara na uwekezaji hugusa **haki nyingi za msingi za binadamu** ikiwa ni pamoja na haki ya kupata afya bora, ulinzi binafsi, ulinzi wa kijamii, uhuru wa kujieleza, ajira, kumiliki mali na maisha bora.

Kuzingatia **mifumo iliyopo yenye kusimamia haki** (kwa mfano juu ya kazi, ardhi na mazingira) ni hatua muhimu katika kukuza haki za binadamu. Kama ambavyo tafiti juu ya haki za kazi kwenye viwanda vya kuchakata samaki vilivyochaguliwa kwa ajili ya utafiti Mwanza na shamba la maua Arusha zinavyoonesha, uzingatiaji wa viwango vya kazi hupunguza mazingira magumu ya kazi na kuleta fursa bora za uchumi. Kinyume chake, kujali kiasi au kutojadili kabisa kunaweza kusababisha mazingira yatakayosababisha ukiukwaji mkubwa sana wa haki. Tafiti juu ya kijiji cha Uvinje / Hifadhi ya Taifa ya Saadani na Msitu wa Makere zinaonesha mifano tosha ya uminywaji wa haki za binadamu, ikiwa ni pamoja na uharibifu wa mali binafsi, unyang'anyaji ovyo wa ardhi na matumizi makubwa ya nguvu, ambayo yanasababishwa na kutotii kanuni za umiliki wa ardhi na uhifadhi wa maliasili. Hivyo basi, kuna umuhimu mkubwa wa kuwa na mifumo thabiti ya kisheria, ambayo inajitosheleza (yaani haiweki utengamano kati mamlaka

mbalimbali) na ambayo ufuatiliaji na utekelezaji wake ni wa kifanisi. Kama ambavyo chunguzi kifani zilionesha kwenye chapisho hili, kuna umuhimu mkubwa wa kuongeza ufanisi. Tafiti hizi zitachochea utekelezaji wa Dola kutimiza *wajibu* wake wa *kulinda* haki za binadamu na wa makampuni *kuheshimu* haki za binadamu (yaani Nguzo ya 1 na ya 2 ya Miongozo ya Umoja wa Mataifa juu ya Biashara na Haki za Binadamu (UNGPs)).

Ujumbe mwingine muhimu ni namna **haki za binadamu zinatiliwa umaanani** – au hatua zinazochukuliwa katika kuainisha, kuzuia, kupunguza na kuweka kumbukumbu sahihi za athari zilizokithiri za haki za binadamu[5] – inathibitisha sharti muhimu katika kuzuia haki za binadamu zisiminywe. Katika kutathmini kwa ufanisi athari za kimazingira na za kijamii, Kuhakikisha uwepo wa ushiriki wa juu na wazi, huru na kupewa taarifa ya ridhaa kutoka kwa wale watakaokuwa wameathirika zaidi na biashara au uwekezaji, na kuweka mbinu thabiti za kufanya maridhiano ni baadhi ya hatua muhimu zilizowekwa kwenye toleo hili la tafiti za "*Sauti za Watanzania"*. Uchunguzi kifani wa Kijiji cha Uvinje ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Saadani unaonesha ambavyo kutotekeleza vema haki za binadamu kabla ya uwekezaji kwenye utalii kumechangia moja ya migogoro mirefu ya ardhi Tanzania. Utafiti juu ya mambo yanayohusisha haki za binadamu kwenye ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki pia unasisitiza umuhimu wa kuwa na michakato sahihi ili kulinda haki za binadamu kwenye mradi huu wa ujenzi kabambe wa miundo mbinu. Kwa kuongezea, tafiti zote tano zinaonesha wazi mbinu za kupunguza na kuboresha haziko sawa na zinatumika chini ya kiwango. Hivyo, **kupata maridhiano** (nguzo ya 3 ya Miongozo ya Umoja wa Mataifa juu ya Biashara na Haki za Binadamu), kunaendelea kuwa changamoto.

Mwisho, ingawa si kwa umuhimu – na ingawa kuna utofauti wa kijiografia na kimada -, tafiti zote tano kwenye *"Sauti za Watanzania"* zinaleta hitimisho hili jumuishi: **kukuza uelewa** juu ya miongozo ya msingi ya ya biashara na haki za binadamu– ikiwa ni pamoja na namna ya kupata maridhiano kikamilifu – ni jambo la lazima katika katika kutekelezaji wa haki za binadamu kwa wote Tanzania.

Mapendekezo kutokana na chapisho hili la tafiti za *"Sauti za Watanzania"* ni pamoja na:

- **Kujenga uwezo** na **kukuza uelewa wa biashara na haki za binadamu** na wadau wote Tanzania, ikiwa ni pamoja na waajiriwa, waajiri, wawekezaji, wafanyakazi serikalini, wadau wa asasi za kiraia, na umma kwa ujumla;
- Kuweka mifumo thabiti ya sheria na kanuni za kutekeleza **haki za binadamu kwa umakini** kwenye shughuli zote za biashara na uwekezaji;
- Kuhakikisha **ushiriki wa makundi yote**, ikiwa ni pamoja na wanawake, vijana, wazawa na makundi ya wasiojiweza kwenye michakato ya kutoa ushauri na kufanya maamuzi juu ya biashara na uwekezaji;
- **Kuweka mifumo ya kikanuni na mamlaka** za watawala kuondoa mapungufu, mkanganyiko na kukosekana kwa ufanisi;
- Kuendeleza na kusaidia **usimamizi sahihi na huru** wa uzingatiaji wa haki za binadamu;
- Kutoa **rasilimali za kutosha**, za fedha na nguvu kazi, kwa wakala wa serikali waliopewa mamlaka ya kufuatilia uzingatiaji wa sheria na kanuni;
- Kuboresha **upatikanaji wa nafuu za kisheria** kwa wote, endapo haki za binadamu zitavunjwa.

5 Angalia kwa mfano https://www.business-humanrights.org/en/un-guiding-principles/implementation-tools-examples/implementation-by-companies/type-of-step-taken/human-rights-due-diligence

"Sauti za Watanzania" ni ushirikiano baina ya asasi za kiraia za Tanzania, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (CHRAGG), Asasi ya Biashara na Haki za Binadamu Tanzania (BHRT) na Shirika la IPIS. Chapisho hili ni sehemu ya mradi wa '**Uboreshaji wa ufuatiliaji, tafiti na majadiliano juu ya Biashara na Haki za Binadamu Tanzania**' unaotekelezwa na CHRAGG, BHRT na IPIS, unaofadhiliwa na Umoja wa Ulaya, Kitengo kinachoshughulikia Demokrasia na Haki za Binadamu (EIDHR).

Mawasiliano: bizhumanrightsTanzania@gmail.com